

ZIARA YA KAMATI YA MIPANGOMIJI NA MAZINGIRA

Tarehe 12. 10. 2023, Kamati ya Mipangomiji na Mazingira, ya Manispaa ya Morogoro, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mwembesongo, Mheshimiwa Ally Rashid Kalungwana, imetembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari, kwenye Kata ya Ruhungo, ujenzi wa soko la machinga kwenye Kata ya Sabasaba, eneo ambalo Kliniki ya Hakimi iliyopo Kata Kilakala imeomba ilitumie kupanua huduma zake, na eneo lililotolewa na wananchi wa Kata ya Chamwino kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari.

Kamati imefurahishwa na kasi ya ujenzi wa shule mpya katika kata ya Ruhungo, na imempongeza Mkurugenzi wa Manispaa pamoja na timu yake ya wataalamu kwa kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ubora zaidi kwa manufaa ya wananchi wa Morogoro na jamii ya Watanzania kwa ujumla.

Aidha, Kamati imewapongeza wananchi wa Kata ya Chamwino kwa kuamua kujitolea maeneo yao ili kupisha ujenzi wa shule mpya ya sekondari kwani kitendo hicho kimeonesha moyo mzuri wa shauku ya maendeleo ambao wananchi wa Chamwino wanao, na kuahidi kuunga mkono juhudi hizo.







MWISHO